**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU UAMUZI WA RUFAA DHIDI YA UAMUZI WA WASIMAMIZI WA UCHAGUZI KWA PINGAMIZI ZA UTEUZI WA WAGOMBEA UBUNGE KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO NA UDIWANI KWA TANZANIA BARA

**Dodoma, Tarehe 31 Agosti, 2025**

Kwa mujibu wa kifungu cha 53 na 65 vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, baada ya uteuzi kufanyika, wagombea Ubunge na Udiwani wanaruhusiwa kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi.

Kifungu cha 53(6) na 65(7) vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 vikisomwa pamoja na kanuni ya 29(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 vinaeleza kuwa, mgombea yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi kuhusu uhalali wa pingamizi lililowekwa anaweza kukata rufaa kwa Tume ndani ya saa ishirini na nne tangu uamuzi ulipotolewa. Tume inaweza kukataa au kukubali rufaa husika wakati wa kufanya uamuzi.

Kwa kuzingatia masharti ya vifungu tajwa vya Sheria, hadi kufikia tarehe 31 Agosti, 2025 zimepokelewa rufaa 33, kati ya rufaa hizo, rufaa 13 zimefanyiwa uamuzi na Tume, ambapo kati yake rufaa nane (08) ni za kupinga uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi kuhusu Ubunge na rufaa tano (05) ni kupinga uamuzi kuhusu Udiwani.

Katika kikao chake maalum kilichofanyika leo tarehe 31 Agosti, 2025, Tume imezikubali rufaa mbili (02) na kuzikataa rufaa (06) za ubunge na imekubali rufaa mbili (02) na kuzikataa rufaa tatu (03) za udiwani kama ifuatavyo:

**1. Rufaa ubunge zilizokubaliwa:**

Zifuatazo ni Rufaa mbili (02) za wagombea ubunge zilizokubaliwa:-

i. **Ndugu Ezekiel Gabriel Katabi** mgombea ubunge Jimbo la Muhambwe kupitia Chama cha CHAUMMA dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Muhambwe; na

ii. **Ndugu Athuman Issah Henku** mgombea ubunge Jimbo la Ikungi Mashariki kupitia Chama cha CUF dhidi ya Ndugu Thomas Mgongo Kitima mgombea ubunge kupitia Chama cha Mapinduzi.

Hivyo, wagombea tajwa, wamerejeshwa katika orodha ya wagombea ubunge katika majimbo husika na waendelee na taratibu za kampeni za uchaguzi.

**2. Rufaa ubunge zilizokataliwa:**

Zifuatazo ni Rufaa sita (6) za wagombea ubunge zilizokataliwa-

i. **Ndugu Msowoya Gelard Goodluck** mgombea ubunge Jimbo la Kilombero kupitia Chama cha ACT - WAZALENDO dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Kilombero;

ii. **Ndugu Innocent Gabriel Siriwa** mgombea ubunge Jimbo la Kibamba kupitia Chama cha ADC dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Kibamba;

iii. **Ndugu David January Mhanga** mgombea ubunge Jimbo la Mkuranga kupitia Chama cha CHAUMMA dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Mkuranga;

iv. **Ndugu Christina Gasper Mbise** mgombea ubunge Jimbo la Ubungo kupitia Chama cha ADC dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Ubungo;

v. **Ndugu Cecil Fransis Akili** mgombea ubunge Jimbo la Ndanda kupitia Chama cha ACT-WAZALENDO dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Ndanda; na

vi. **Ndugu Mneke Jafari Saidi** mgombea ubunge Jimbo la Newala Vijijini kupitia Chama cha CUF dhidi ya Ndugu Nawanda Yahaya Esmail mgombea ubunge Jimbo la Newala Vijijini kupitia Chama cha Mapinduzi;

Hivyo, kwa wagombea kuanzia namba namba ***i*** ya kirumi hadi namba ***v*** ya kirumi, Tume imekubaliana na uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo husika wa kutowateua kugombea nafasi ya ubunge katika majimbo husika.

Aidha, kwa mrufaniwa namba ***vi*** ya kirumi ya Ndugu Nawanda Yahaya Esmail, Tume imekubaliana na uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi wa Jimbo la Newala Vijijini, hivyo aendelee na taratibu za kampeni za ubunge.

**3. Rufaa za udiwani zilizokubaliwa:**

Zifuatazo ni Rufaa mbili (02) za wagombea udiwani zilizokubaliwa:-

i. **Ndugu Yasini Mazoea Bakiri** mgombea udiwani Kata ya Mlingula Jimbo la Ndanda kupitia Chama cha ACT-WAZALENDO dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Ndanda; na

ii. **Ndugu Alex Tresiford Nachingulu** mgombea udiwani Kata ya Mwena Jimbo la Ndanda kupitia Chama cha ACT-WAZALENDO dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Ndanda.

Hivyo, wagombea tajwa, wamerejeshwa katika orodha ya wagombea udiwani katika kata husika na waendelee na taratibu za kampeni za uchaguzi.

**4. Rufaa za udiwani zilizokataliwa:**

Zifuatazo ni Rufaa tatu (03) za wagombea udiwani zilizokaliwa:-

i. **Ndugu Abisai Raston Hankungwe** mgombea udiwani Kata ya Mabatini Jimbo la Mbeya Mjini kupitia Chama cha CHAUMMA dhidi ya Ndugu Stephen Kael Mwaisumo mgombea udiwani Kata ya Mabatini kupitia Chama cha Mapinduzi; na

ii. **Ndugu Mwajuma Hamidu Tito** mgombea udiwani Kata ya Nanganga Jimbo la Ndanda kupitia Chama cha CUF dhidi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Kata ya Nanganga Jimbo la Ndanda.

iii. **Ndugu Jacob Jaston Mdolo** mgombea udiwani Kata ya Ilolo Jimbo la Vwawa kupitia Chama cha Mapinduzi dhidi ya ndugu Richard Mwendanjila Kibona mgombea udiwani Kata ya Ilolo kupitia Chama cha CHAUMMA;

Hivyo, kwa wagombea namba ***i*** na ***ii*** za kirumi, Tume imekubaliana na uamuzi ya wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi wa kata husika wa kutowateau kugombea nafasi ya udiwani.

Aidha, kwa mrufaniwa namba ***iii*** ya kirumi Ndugu Richard Mwendanjila Kibona, Tume imekubaliana na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Kata ya Ilolo, hivyo aendelee na taratibu za kampeni za udiwani.

Aidha, Tume itaendelea kutoa taarifa kwa Umma kuhusu uamuzi wa rufaa kwa kadri itakavyokuwa inazipokea.

***"KURA YAKO HAKI YAKO JITOKEZE KUPIGA KURA"***

Imetolewa na:

Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**